TANGAZO LA SERIKALI Na. 51Q la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA. 332)

## AMRI

*(Imetengenezwa chini ya Kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA YA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA KIFEDHA ZA NJE KATIKA MRADI WA UZALISHAJI MBOLEA ZA ASILI KWA KAMPUNI YA ITRACOM FERTILIZER YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Riba ya Mikopo Kutoka Taasisi za Kifedha za Nje Katika Mradi wa Uzalishaji Mbolea za Asili kwa Kampuni ya Itracom Fertilizer ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 22 Juni, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio kwenye riba ya mikopo kutoka taasisi za kifedha za nje kwa ajili ya mradi wa uzalishaji mbolea ya Kampuni ya Itracom Fertilizer imesamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo tarehe 21 Juni, 2028 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Itracom Fertilizer na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 5 Aprili, 2022.

Dodoma
31/12/2024

**MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU**
*Waziri wa Fedha*